Utangulizi

● Namna ya kutumia kitabu hiki cha nyongeza

Kitabu hiki ni cha kujifundishia Sehemu ya Tatu ya mafunzo ya Kijerumani kwa Redio: *Deutsch – warum nicht?* Kama Sehemu ya Kwanza na ya Pili, kimekusudiwa kuwa kitabu cha marudio, wala hakikukusudiwa kuwa kitabu cha kujifunzia mwenyewe. Jaribu kila mara kusikiliza mafunzo yenyewe redioni kabla hujakifungua kitabu hiki.

Mazoezi ya kusikiliza kila somo redioni yatakusaidia kufahamu vyema zaidi yote yaliyo muhimu. Hii ni kumaanisha kuwa ufahamu kwa jumla yale yanayotokea, mifano inaonyeshwa wapi, nani anazungumza na nani, wahusika wanazungumza nini, na hali zao ziko vipi. Jaribu kuyashughulikia yote haya, na kumbuka kuwa si lazima ufahamu neno kwa neno.

● Nini kipya katika Sehemu ya Tatu?

Wahusika muhimu katika mafunzo haya ya lugha watasikika tena katika Sehemu ya Tatu:

- **Andreas** ni mwanafunzi na baadhi ya wakati wake anafanya kazi ya mpokezi katika Hotel Europa.
- **Ex** ni kijizimwi jike kutoka mawazoni tu. Hawezi kuonekana kwa macho, lakini sauti yake inasikika vizuri. Alitoweka mwishoni mwa Sehemu ya Pili ya mfululizo wetu, lakini sasa amerudi tena.

Wahusika wengine muhimu wamekwisha mzowea yeye pamoja na namna yake ya kuzungumza nao ...

- **Dr. Thürmann** anaishi Berlin, lakini ni mgeni wa mara kwa mara katika Hotel Europa.
- **Frau Berger** ni Meneja wa hoteli.
- **Hanna Clasen** ni msichana anayesafisha vyumba hotelini.

Muundo wa masomo ni ule ule kama katika Sehemu ya Kwanza na ya Pili. Kwanza utasikia mazungumzo, kisha maelezo yake. Baadae itafuata sehemu ya sarufi, kisha mazungumzo yatarudiwa tena.

Mazungumzo katika Sehemu ya Tatu ni magumu kidogo yakilinganishwa na sehemu mbili za kwanza za mfululizo huu.

Wakati Sehemu ya Kwanza na ya Pili zilitokea **Aachen**, nusu ya pili ya Sehemu ya Tatu inatokea **Berlin**. Katika nusu hiyo ya pili, masomo yanatoa habari kuhusu jiji hilo na Historia yake. Utasikia hadithi kuhusu Berlin zitakazokusaidia uufahamu kidogo mji huo.

Mwanzoni mwa Sehemu ya Tatu tunakujulisha tena wahusika muhimu. Pia inarudiwa miundo muhimu kabisa ya sarufi ili uweze kuifahamu sehemu hii hata kama bado hujasikiliza Sehemu ya Kwanza na ya Pili ya mafunzo haya ya lugha.

● Yaliyomo katika Kitabu cha Nyongeza

A Habari kuhusu Historia ya Ujerumani na Berlin

Muhtasari huu mfupi unatoa habari za kimsingi kuhusu Historia ya Ujerumani ambayo toka 1945 mpaka 1990 iligawanywa katika Ujerumani ya Magharibi (Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani) na Ujerumani ya Mashariki (Shirikisho la Kidemokrasi la Ujerumani).

B Habari kuhusu kila somo

1. Muhtasari wa sarufi

Humu unatolewa muhtasari wa sarufi na maana ya vifungu vya maneno kutoka kila somo. Sarufi inaelezwa kwa ufafanuzi, kwa kutolewa mifano kutoka kila somo. Vifungu vya maneno vimeorodheshwa kwa Kijerumani – na siyo kwa Kijerumani na Kiswahili kama katika **(unaweza kutumia yafuatayo)** Sehemu ya Kwanza na ya Pili. Ilipowezekana, vifungu hivyo vya maneno vimeorodheshwa kufuatana na muundo na namna ya utumizi wake katika kila somo, ijapokuwa vimeorodheshwa pia kufuatana na orodha ya kamusi.

Mfano:

Sentensi ifuatayo, *Sie singt gern* imeorodheshwa pia katika muundo wa kitenzi jina (infinitive): *etwas gern tun.* Hii inakuwezesha kutunga sentensi nyingine kwa kutumia muundo huu huu, kwa mfano: *Er liest gern.* Ikiwa hujafahamu maana ya kifungu maalumu, unaweza kutafuta maana yake katika tafsiri ya mazungumzo mwishoni mwa kitabu. Na masomo kuhusu Berlin yana habari maalumu kulihusu jiji hilo na namna linayowavutia watalii.

2. Maandishi katika kila somo

Maandishi – ikiwa ni katika muundo wa mazungumzo, habari muhimu, barua au nyimbo – yameandikwa kwa Kijerumani baada ya muhtasari wa sarufi na vifungu vya maneno. Ili kukuwezesha ufahamu kwa wepesi, maandishi hayo yametanguliwa na maelezo mafupi kwa Kiswahili. Kwa hivyo ukikosa kusikiliza somo moja redioni, unaweza kulifuatilia katika kitabu.

3. Maneno na vifungu vya maneno

Ni vifungu na maneno yale tu yanayotumiwa hapa kwa mara ya kwanza, yanayoorodheshwa katika kila somo. Lakini maneno mapya ambayo, kwa mfano, yanatumiwa katika maandishi ya msanii *Bert Brecht,* hayakuorodheshwa. Pia, hayakutumiwa maneno na vifungu vya maneno kutoka sehemu ya Kwanza na ya Pili ya mafunzo ya Kijerumani.

4. Sehemu kubwa ya mazoezi inaelezea sarufi, lakini yako pia mazoezi ya maneno na maana yake, kwa mfano kujaza jadwali ya maneno, pamoja na matumizi sahihi ya maneno na vifungu vya maneno. Pia sehemu ya tatu ina mazoezi ya ufahamu (comprehension). Kwa mfano unaweza kuona orodha ya misemo (phrases) au sentensi na ukatakiwa uchague vifungu vya maneno ulivyovisikia katika mafunzo ya redioni. Panapohitajika, unaweza kutazama kwenye mazungumzo yaliyochapishwa kikamilifu katika kila somo. Mara kwa mara utatakiwa uangalie hasa kwenye mazungumzo haya. Majibu ya sehemu kubwa ya mazoezi utayakuta katika ufafanuzi wa mazoezi mwishoni mwa kitabu. Kila penye uwezekano wa kutolewa zaidi ya jibu moja, hutolewa mifano kadha ya majibu katika ufafanuzi wa mazoezi na kuwekewa alama kama hii: ** Ufafanuzi wa mazoezi hautoi majibu kwa maswali unayotakiwa ujibu kwa maneno yako mwenyewe.

C Muhtasari wa sarufi

Hapa pametolewa muhtasari wa sarufi mpya katika Sehemu ya Tatu. Sarufi muhimu katika Sehemu ya Tatu ni:

1. Wakati uliopita (imperfect tense) wa vitendo vya kawaida na visivyo vya kawaida (regular and irregular verbs) pamoja na vitendo vya utaratibu (modal verbs).
2. Viunganisho vya sentensi:
   Viunganisho muhimu vya sentensi mbili, kwa mfano, ni: *und, aber, sondern*
   Viunganisho vinavyotumiwa kuunganisha kitenzi kikuu na kitenzi kisaidizi, kwa mfano *daß, weil*
3. Mwendesho (declension) wa vivumishi vya sifa (adjectives)

D Ufafanuzi wa mazoezi

Ufafanuzi wa mazoezi unatumiwa kuhakikisha iwapo umetoa majibu sahihi kwa mazoezi kutoka kila somo.

E Tafsiri ya mazungumzo

Tafsiri ya mazungumzo imekusudiwa kukusaidia ufahamu lugha kwa urahisi zaidi, hasa ikiwa hukuweza kujiunga nasi katika Sehumu ya Kwanza na ya Pili, na hujui maana ya maneno na sarufi iliyokwisha elezwa. Kufuatana na haki za kunakili, maandishi halisi kutoka nyimbo na tenzi hayakuchapishwa katika kitabu hiki.

F Orodha ya maneno kwa mujibu wa alfabeti

Humu utayakuta maneno yote mapya yaliyotumiwa kwa mara ya kwanza katika Sehemu ya Tatu. Maneno yaliyotumiwa katika Sehemu ya Kwanza na ya Pili hayakuorodheshwa hapa. Namba iliyowekwa ndani ya mabano (brackets) hukukumbusha somo lilimotumiwa, neno au kifungu cha maneno.

G Orodha ya vitendo: Kitenzi jina (infinitive) – wakati uliopita (imperfect tense) – kitenzi cha tendo kamilifu (past participle)

Katika orodha hii utakutana na vitendo vyote vilivyotumiwa katika Sehemu ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu ya mafunzo haya. Kitenzi jina, wakati uliopita na kitenzi cha tendo kamilifu, imetolewa kukuwezesha kutunga nyakati (tenses) muhimu kabisa.

Mfano: *kommen – kam – gekommen <sein>*

Kitenzi jina: *kommen*

Wakati uliopita: *(er/sie) kam*

Kitenzi cha tendo kamilifu: *gekommen*

sein imewekwa katika mabano kuonyesha kuwa kitendo *kommen* huunda wakati wake kamilifu (perfect tense) kwa kitendo kisaidizi (auxiliary verb) *sein:*

Er ist gekommen.

Huenda umekwisha sikia kuwa mafunzo haya ya Kijerumani yanatangazwa kote duniani katika lugha nyingi mbali mbali. Kwa sababu hii tunasikitika kuwa hatuwezi kuzingatia mambo maalumu yanayoingiza utamaduni na lugha ya nchi yako. Hata hivyo, tunaamini kuwa wewe mwenyewe utakuwa mtu bora kabisa wa kuweza kuamua juu ya tafauti na mlingano uliopo kati ya Kijerumani na lugha yako mwenyewe.

Ni matumaini yangu kuwa utayafurahia masomo haya na kwamba utafanikiwa na mafunzo haya ya *Deutsch – warum nicht?*

Herrad Meese

Habari muhimu

1 Historia ya Ujerumani

Ufuatao ni muhtasari tu wa Historia ya Ujerumani. Madhumuni yake ni kukupa habari za kimsingi kuhusu vipindi vya nyakati maalumu katika Historia ya nchi hii ili uweze kufahamu kwa wepesi zaidi baadhi ya masomo katika Sehemu ya Tatu ya mafunzo haya. Nyakati hizi tumezichagua ili kutilia mkazo yale mambo yaliokuwa chanzo cha kuundwa utambulisho wa kitaifa nchini Ujerumani.

919: kuundwa kwa dola la kwanza la Kijerumani

Mnamo karne ya 19: Ujerumani ni mwungano wa mikoa kadha

Mnamo karne ya 19 Ujerumani ilikuwa mwungano wa mikoa binafsi – mali ya wafalme, wana wafalme au jamaa zao. Kwa namna zao, watawala wa mikoa hii mingi, walikuwa ni watu wenye nguvu. Hata hivyo, kuanzia karne ya 19 kukaanza kuzuka hisia ya umuhimu wa kuweko utambulisho wa kitaifa.

1871–1918: Kuundwa kwa Dola la Pili la Kijerumani la Kaizari

1870/71: Vita kati ya Ufaransa na Ujerumani
1871: Kuundwa kwa Dola la Pili la Ujerumani la Kaizari kwenye kasri la Versailles. William I. atawazwa kuwa Mfalme Ujerumani. Berlin unachaguliwa kuwa mji mkuu
1918: Kuanguka kwa Dola la Kaizari mwisho wa Vita vikuu vya kwanza vya Dunia

1919–1933: Jamhuri ya Weimar

1919: Katiba ya Weimar
1919: Kutiwa saini Mkataba wa amani wa Versailles

1933–1945: Usoshalisti wa Kitaifa (National Socialism) Dola la Tatu la Kijerumani

1933: Adolf Hitler anaapishwa kuwa Kansela
1939: Ujerumani yaivamia Poland; kuanza kwa Vita Vikuu Vya Pili vya Dunia
1945: Ujerumani inasalimu amri kabisa. Mwisho wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia. Madola yaliyoshinda vita, Marekani, Umoja wa Soviyeti, Ufaransa na Uingereza, yanaigawa sehemu nne Ujerumani. Matokeo ya Vita hivyo, ni kugawanywa sehemu mbili nchi ya Ujerumani

1949–1990: Ujerumani imegawanywa katika nchi mbili za Kijerumani: Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani (Ujerumani ya Magharibi) na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Ujerumani (Ujerumani ya Mashariki)

1949: Kuundwa kwa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani. Bonn unafanywa mji mkuu; Ujerumani inajiunga na NATO
1949: Kuundwa kwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Ujerumani. Berlin ya Mashariki unafanywa mji mkuu. Ujerumani ya Mashariki yajiunga na Mkataba wa Warsaw

Tokea wakati huo, Ujerumani iligawanywa – kama vile jiji la Berlin. Mwanzoni, raiya wa Ujerumani ya Magharibi hawakuweza kuitembelea Ujerumani ya Mashariki, na ilikuwa haiwezekani kabisa kwa raiya wa Ujerumani ya Mashariki kuhamia Ujerumani ya Magharibi. Walioruhusiwa kuhamia iliwabidi kwanza wafikie umri wa kustahafishwa.
Baina ya 1945 na 1957, watu milioni 2.7 (au asili miya 15 ya raiya wa Ujerumani ya Mashariki) walikimbilia Ujerumani ya Magharibi. Wengi wao walikuwa wafanya kazi wenye ujuzi muhimu wa kazi. Kuanzia 1961, mpaka baina ya Ujerumani ya Mashariki na ya Magharibi ulifungwa kwa ukuta na waya za senyenge na kuwekewa ulinzi mkali: Askari wa mipakani wa Mashariki walipewa amri kumpiga risasi yeyote yule anayejaribu kutorokea Magharibi. Mwaka huo huo ukajengwa Ukuta wa Berlin kuitenga kabisa Berlin ya Mashariki na Magharibi.

3.10.1990 : Mwungano wa Ujerumani Magharibi na Mashariki

Tangu 1990 Ujerumani ni nchi moja. Berlin umechaguliwa tena kuwa mji mkuu, na Bonn utabakia kuwa makao rasmi ya kiserikali kwa muda wa mpito.

2 Historia ya Berlin

1470: Berlin wafanywa makao ya Mwana-Mfalme Mteule wa Brandenburg
1709: Berlin wafanywa mji mkuu wa Mamlaka ya Ufalme wa Prussia
1871: Berlin wafanywa mji mkuu wa Dola la Ujerumani
1939: Mwanzo wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia
1945: Mwisho wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia
Berlin unatawaliwa na "Madola Manne Makuu" (Uingereza, Ufaransa, Marekani na Umoja wa Sovieti)
1946: Uchaguzi huru wafanywa kote Berlin

Berlin – mji uliogawanywa toka 1948–1989

1948: Berlin wagawanywa katika sehemu mbili, Mashariki na Magharibi
1948/49: Berlin wazingirwa
Wasovieti wanafunga njia zote za kuingilia na kutokea Berlin, yaani walizuiya usafiri na huduma zote za upelekaji bidhaa kwa jiji hilo. Kwa muda wa mwaka mzima madola shirika ya Magharibi yalipeleka Berlin bidhaa na chakula kwa ndege.
1953: Machafuko ya kupinga utawala wa Ujerumani ya Mashariki.
1958: Krushchev anatangaza Mapatano ya Madola Manne na anadai kuwa Berlin ya Magharibi ufanywe mji huru.
1961: Ukuta wa Berlin unajengwa kuugawa pande mbili mji wa Berlin. Raiya wa Berlin ya Magharibi hawawezi tena kuvuka mpaka na kuenda Berlin ya Mashariki. Mbali na ukuta, unasimamishwa mpaka mpana wenye kulindwa vikali. Yeyote anayejaribu kukimbilia Berlin ya Magharibi anapigwa risasi.
1963: Mapatano ya kwanza yanafanywa kuwaruhusu raiya wa Berlin ya Magharibi kuwatembelea jamaa zao Berlin ya Mashariki kila mwisho wa mwaka.
1968: Raiya wa Ujerumani ya Magharibi wanahitaji Pasi kwa safari ya kuenda Berlin ya Magharibi na wanahitaji pia Viza kuingia Ujerumani ya Mashariki.
1989: Ukuta una funguliwa na Lango la Brandenburg linafunguliwa kuwaruhusu raiya wa Berlin ya Mashariki na Magharibi kutembeleana huru na kuenda kokote watakako jijini.
1990: Ukuta wa Berlin unabomolewa.

3 Ramani ya Berlin

4 Miezi katika mwaka

1	Januar	Januari	7	Juli	Julai
2	Februar	Februari	8	August	Agosti
3	März	Machi	9	September	Septemba
4	April	Aprili	10	Oktober	Oktoba
5	Mai	Mei	11	November	Novemba
6	Juni	Juni	12	Dezember	Disemba

Wann kommen Sie? Im Januar.

5 Mwelekezo wa dira

der Norden / Kaskazini
nördlich / Upande wa kaskazini

Der Westen / Magharibi
westlich / Upande wa Magharibi

Der Osten/ Mashariki
östlich / Upande wa Mashariki

Der Süden / Kusini
südlich / Upande wa Kusini

Wo liegt Aachen? Aachen liegt im Westen (von Deutschland).
Wo liegt Köln? Köln liegt nördlich von Bonn.
Köln liegt nordöstlich von Aachen.

Man ging durch das Brandenburger Tor von Osten nach Westen.
Berlin kann eine Brücke zum Osten werden.

6 Namba kutoka 100 mpaka 1,000

100 = hundert	500 = fünfhundert	800 = achthundert
200 = zweihundert	600 = sechshundert	900 = neunhundert
300 = dreihundert	700 = siebenhundert	1000 = tausend
400 = vierhundert		

101 = einhunderteins 202 = zweihundertzwei 311= dreihundertelf
420 = vierhundertzwanzig 435 = vierhundertfünfunddreißig

100. = **Nominative:** Das ist der hundertste Geburtstag,
das ist die hundertste Frage,
das ist das hundertste Buch.

Accusatve: Er hat den hundertsten Geburtstag,
er stellt die hundertste Frage,
er kauft das hundertste Buch.

7 Tarehe

Namba mbili za mwanzo kuanzia kushoto ni karne. Ukitaka kutaja mwaka, unaongezea neno miya = *hundert* baada ya namba hizo kama katika Kiswahili. Kwa mfano:

911 = neunhundertelf
1871 = achtzehnhunderteinundsiebzig
1961 = neunzehnhunderteinundsechzig
1990 = neunzehnhundertneunzig